www.eeducationgroup.com

# MTIHANI WA KABLA YA MWIGOI 2015

## INSHA.

1 MWONGOZO KARATASI LA KWANZA

1) Anwani ya Mwandishi
2 Mada. – Herufi kubwa na ipigiwe mstari
Mada itaje ni risala kwa nani kwa nani na ~~g~~ kuhuso nini.

3. Mtajo utategemea mwandikiwa
mf Kwa rais na wananchi wa....
wazalendo wa...
raia ...
watu wa ....
4. Utangulizi – Uonyeshe masikitiko. Ihuzuni nk.

5 Mwili
→ Changamoto za kigaidi
→ Namna mataifa yanakabiliana na ugaidi
→ Kisa cha mashambulizi katika nchi zingine.
→ Kuhimiza taifa hilo kujasirika /Kutia moyo. /
→ Kutia juhudi na mikakati dhidi ya ugaidi
→ → Uhamaji /suala la wakimbizi
→ mashirika yasiyo ya kiserekali
→ Usalama katika nyanja na sehemo zilizo na ~~wananch~~ watu wengi
→ Benki bandia – kupitisha fedha.
– Kutoa msimamo wake kuhuso ~~& soluh~~ swala hilo. /Mo – Asisitize msimamo wake.
(6) Hitimisho
– Jina lake na sahihi kuandikwa.

# DHULUMA DHIDI YA MWANAMKE

1. Kichwa
Herufi kubwa na ipigiwe kistari
- ~~Ele~~

2. Utangulizi
Kueleza maana ya dhuluma na kutolea mifano mbalimbali.

3. Mwili
→ Kujadili hoja
   1. Ukeketaji
   2. Ndoa za mapema
   3. Kuvuliwa nguo hadharani
   4. Kubezwa na kudharauliwa hadharani
   5. Ubakaji
   6. Kupigwa na waume
   7. Kudhulumiwa kazini - Kimapenzi
      Kupuuzwa
      Kunyimwa vyeo
      Majukumu mengi
   8. Kutengwa katika ~~kort~~ kurithi mali hasa wajane.
   9. Jamii hutenga ~~wa~~ wasichana kielimu.
   10. Nafasi za kazi.
   ~~Na A Tahi~~
   Hakiki mifano mingine.

Hoja zisipungue sita.
Maneno 400.

MZIGO WA MWENZIO NI KANDA LA USUFI

3

Methali

① Kichwa → Kiandikwe katika herufi kubwa na kipigiwe kistari
- Yaweza kuwa sehemu ya methali au kudokeza methali hiyo. mf mzigo wa mwenzio

② Utangulizi
- Anaweza kutoa maana ya juu na ndani ya methali na matumizi ya methali
- Anaweza buni kisa ~~Aa~~ ambacho kinadhihirisha pande mbili za methali
① Nani alikuwa na tatizo (mzigo)
② Aliyepuuzilia mbali tatizo hilo (kanda la usufi)
③ Makundi mawili yajitokeze.

Hitimisho
- Muktasari wa kisa.
- Funzo lidhihirike la methali husika.

Maneno 400 -

www.eeducationgroup.com

(4) Na huo ukawa mwanzo mpya.

(1) Kichwa.

Mwanafunzi abuni kichwa cha Insha.

(2) Mwili

- Atunge kisa kinachohusiana na kichwa na kilichotolewa.
- Atumia lugha ya mvuto mkubwa.
- Kuwepo na mtiririko mzuri wa kisa husika.

(3) Hitimisho

Amalizie Insha kwa maneno aliyopewa, bila kuongeza wala kudondoa.

- Asipomalizia au aongeze apate bakshishi

02/20

**KARATASI 102/2**
**KIDATO CHA NNE**

# MWONGOZO

**Maagizo:**

**Jibu maswali yote. Majibu yako yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa.**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| UFAHAMU | 15 | |
| UFUPISHO | 15 | |
| SARUFI | 40 | |
| ISIMU JAMII | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

**UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.**

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na uathihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu msingi mkuu wa uainishaji wa mahusiano hayo ni kukichunguza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano baina ya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache, na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitikadi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hivyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huu hautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu; tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi, kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi, na kudumisha uhusiano wetu wa kijamaa. Hata hivyo, inawezekena baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au kipindi kirefu, unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili, mahusiano ya koindi cha wastani, kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mwahali mwa kazi, washirika kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekana kudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya, hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfano wa jamii. Kwa mfano, kwa majirani wanaoishi kwenye janibu, fulani mahususi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri. Uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilkikabadilika. Isitoshe, kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari **yameghoshi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi uweza kuumomonyoa ukuta wa uhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano kati ya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wa majirani. Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasa huweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujiri katika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa dukani, kwenye sehemu za ibada, kwenye kituo cha mafuta, kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mapito. Kwanza, uwezekano wa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi untambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na "uhusiano wa chembe chembe". Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachomshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, kiatu anachokushonea, nguo anazokufulia, ususi anaokufanyia n.k. Mahusiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisasa na kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwenzake kwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwezake amekosa chakula, amefutwa kazi, amefiliwa na kadhalika.

Suala kuu tunalopaswa kujiuliza nji: Je, tunahusiana vipi na jamaa zetu, taasisi zetu, marafiki zetu na majirani zetu? Je, uhusiano wetu na raia wenzetu ni w aaina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

(a) Taja kigezo muhimu cha kuzungumzia mahusiano. (al 1)

**Kipindi cha mahusiano yenyewe.**

(b) Eleza imani ya watu kuhusu uhusiano baina ya jamaa. (al 1)

**Ni uhusiano wa kudumu / huchukua muda mrefu / uhusiano wa kipindi kirefu / ni wa milele / huanzia utotoni hadi utu uzima**

(c) Fafanua athari ya technolojia kwenye mahusiano ya watu. (al 2)

**Huwezasha watu au jamaa wako mbali kuwasilianan au hudumisha uhusiano wa kijamii.**

(d) Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo. (al 4)

**(i) Talaka – huvunja uhusiano baina ya mke na mume**
**(ii) Ubadilishija wa kazi**
**(iii) Mifumo ya kimataifa na kisiasa**
**(iv) Mabadiliko ya maisha ya mjini**
**(v) Uhamaji**
**(vi) Kufutwa kazi**

**(zozote x4 x 1 = 4)**

(e) Taja sifa kuu ya mahusiano ya muda mfupi. (al 2)

**Hatuwaliwa na uhusiano wa chembechembe.**

(f) Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? (al 2)

**Mahusiano katika jamii / aina za mahusiano katika jamii.**

(g) Eleza maana ya maneno yafutayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. (al 3)

(i) inasigana **– inapiganan / inakizana / inatofautiana / inahitilafiana**

(ii) yameghoshi **- yamejaa / jamebeba / yamesheheni / yamerundika**

(iii)vighairi **kinyume / vinyume / tofauti**

**UFUPISHO (ALAMA 15)**

Ujambazi wa kimataifa ni tatizo lililowasumbua walimwengu kwa muda mrefu sana. Serikali nyingi zimetumia mapesa mengi kwa miaka mingi sana zikijitahidi kupambana na janga hili. Hata hivyo, fanaka haijapatikana, wala haielekei kamwe kuwa itapatikana leo au karne nyingi baadaye.

Yumkini tatizo kubwa lililopo ni kuhusu jelezi la dhanaya "ujambazi" tena "wa kimataifa". Hili ni tatizo mojawapo na yapo mengi sana. Tatizo la pili ni kiburi. Kuna wale watu binafsi na hasa viongozi w anchi kubwakubwa na serikali zao zilizojiaminisha kuwa ujambaz ni balaa kweli, tena belua, lakini huo ni wa huko, wala hauwezi kuwagusa licha ya kuwashtua wao.

Kulingana na maoni watakaburi hao, ujambazi ni wa watu 'washenzi' wasiostaarabika, wapatikanao katika nchi zisizoendelea bado. Ujambazi peke wanaouona unafaa kukabiliwa ni dhidi ya mbubujiko wa madawa ya kulevya uliosababishwa na vinyagarika kutoka nchi hizo maaluni za "ulimwengu wa tatu". Kulingana na wastaarabu wa nchi zilizoendelea, vinyangarika hivi ndivyo hasa adui mkubwa wa ustaarabu ulimwenguni na ni sharti vifagiliwe mbali bila huruma. Baada ya kusawasagwa, ulimwengu mstaarabu utazidi kutononoka na ahadi ya mbingu hapa ardhini itakamilika.

Imani ya watu hawa ya kuwa ujambazi wa kimataifa, hata iwapo upo, hauwezi kuwashtua wala kuwatingisha wao ilikuwa kamili na timamu. Ilikuwa kamili na timamu hadi hapo mwezi Septemba tarehe 11 mwaka wa 2001, ndege tatu za abiria zilipoelekezwa katika majumba mawili ya fahari, yenye urefu wa zaidi ya ghorofa mia moja na kuyatwangilia mbali. Mshtuko na kimako! Kimako kwa kuwa, kabla ya siku hiyo, Wamarekani hawangeweza kudhani kwamba ingewezekana taifa lolote au mtu yeyote kuthubutu kushambulia nchi yao, taifa wasifa lililojihami barabara dhidi ya aina yoyote ile ya uchokozi kutoka pembe lo lote la dunia.

Hakuna ulimwenguni mzima, aliyeamini kuwa Marekani ingeweza kushambuliwa. Kwa ajili hiyo, mshtuko uliitingisha ardhi yote na huzuni ilitanda kote, kama kwamba sayari nzima imeshambuliwa, wala sio Marekani pekee.

Mintarafu hiyo, Marekani ilipolipiza kisasi kwa kuwaunguza waliokuwemo na wasiokuwemo kwa mabomu hatari huko Afghanistan, idadi kubwa ya watu duniani ilishangilia na kusherehekea. Kwa bahati mbaya, tafsiri ya shambulizi la minara-pacha na Newyork na lile la Pentagon, uti wa uwezo wa kivita wa Marekani, ulizorota. Kuna wengi waliodhani huo ni mwanzo wa vita vya Waislamu dhidi ya Wakristo na kwa muda, Waislamu wote wakashukiwa kimakosa kuwa ni majambazi wa kimataifa.

(a) Bila kubadilisha maana, fupisha aya tatu za kwanza. (maneno 65 – 75) (al 10, 2 za utiririko)
Matayarisho

**a) Ujambazi wa kimataifa umewasumbua walimwengu**

**b) Serikali nyingi zimejitolea kupambana na janga hili**

**c) Fanaka haijapatikana**

**d) Tatizo kubwa ni jelezi la dhana ya ujambazi wa kimataifa**

**e) Tatizo jingine ni kiburi cha mataifa makubwa kuona hayawezi. Kufikwa na ujambazi.**

**f) Kwao ujambazi unaofaa kukabiliwa ni wa dawa za kulevya**

**g) Unasababishwa na vinyang'arika kutoka ulimwengu wa tatu**

**h) Vinyang'rika hizi ni sharti vifangiliwe ili ustaarabu udumishwe.**

**i) Watakaburi hawa wanaamini kuwa ujambazi ni wa watu washenzi katika mchi zisizoendelea.**

**(zozote 7 x 1 = 7, utiririko 1) = alama 8**

(b) Ukizingatia aya tatu za mwisho, fafanua fikira za watu na mambo yote yaliyotokea baada ya Septemba tarehe 11, 2001. (maneno 65 – 75) (al 10, 2 za utiririko)

Matayarisho

**(a) Wamarekaru walishtuka na kumaka kuwa taifa lolote au mtu yeyote angethubutu kuwashambulia**

**(b) Hakuna aliyeamini kuwa marekani ingeweza kushambuliwa**

**(c) Huzuni ilitanda ulimwenguni kote**

**(d) Marekani ulipiza kisasi kwa kuwaunguza waliokuwemo na wasiokuwemo kwa mahomu Afghanistan**

**(e) Wengi duniani walisherehekea**

**(f) Tafsiri ya shambulizi hili ilizorota**

**(g) Wengi walidhani kuwa ulikuwa mwanzo wa vita vya waislamu dhidi ya wakristo.**

**(h) Waislamu wote walishukiwa kimakosa kuwa ni majambazi.**

**Zozote 6 x 1 = 6**

**Utiririko 1**

**7**

**MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

(a) Silabi ni nini? (al 2)

……***Pigo kamili la sauti katika neno***

(b) Tenga silabi katika maneno yafuatayo kisha uandike aina yake. (al 2)

(i) igwa

***i-gwa***

(ii) Oa

***o-a*** Dhihirisha panapotiwa shadda katika maneno yafuatayo. (al 2)

(i) Galaga'la

………………………………………………………………………………………

(ii) Tekete'za ………………………………………………………………………………...

(c) Bainisha nomino katika sentensi zifuatazo kisha utaje aina zake. (al 2)

(i) Uhubiri wa mama huyu una mvuto mkubwa

……***Uhubiri- dhahania*** ……***Mama-kawaida. Mvuto-dhahania***

(ii)Kabati hili limevamiwa na wadudu wengi waharibifu.

***Kabati – kawaida*** ***Wadudu – kawaida*** Eleza matumizi ya kihusishi kwa katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Tahadhari huandikwa kwa hati nzito.

***Jinsi – au chombo/kitumizi***

……………………………………………………………………………………………..

(d) Tenga viambishi na mzizi katika neno lifuatalo. (al 2)

Siji.

***Si-j-i***

……………………………………………………………………………………………..

(e) Unda nomino kutokana na kivumishi kifatacho. (al 1)

Tepetevu

……***Utepetevu***………………………………………………………………………………

Pigia mstari na kuainisha kirai katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Haifai kujenga karubu na nyaya za umeme ***RT***

…***Karibu na –RN*** …***Nyaya za umeme RN***

(f) Bainisha shamirisho kitondo katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Mzalendo amemwandikia mhariri barua.

***Barua-shamirisho kipozi*** ………***Mharir- shamirisho kitondo***

(g) Eleza kama sentensi ifuatayo ni sahili, ambatano ama changamano. (al 2)

Tulipewa ratiba ya shughuli hiyo lakini hatukuitia maanani

**Ambatano: zaidi ya wazo moja**

(h) Bainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Simu tamba ambayo ameninunulia imenirahisishia mawasiliano

***ambayo ameninunulia-kishazi tegemezi***

***Simu tamba imenirahisishia mawasiliano-kishazi huru.***

(i) Kanusha sentensi ifuatayo. (al 2)

Ninamtarajia mpwa wangu awasili leo

***Simtarajii mpwa wangu awasili leo.***

(j) Andika katika wingi. (al 2)

Huzuni aliyokuwa nayo yatima huyu ilinitia kite na imani.

***Huzuni waliyokuwa nayo mayatima hawa ilitutia kite na imani.***

(k) Andika kinyume cha neno lililopigwa mstari. (al 1)

Mhalifu huyu alitunga mimba

***Mhalifu huyu alitungua mimba.***

(l) Bainisha matumizi ya **KI** katika sentensi ifautayo. (al 1)

Jua limekuwa likiwaka tangu Januari

***Hali ya kuendelea.***

(m) Bainisha matumizi ya **ka** katika sentensi ifuatayo: (al 1)

Sungura alifika nyumbani akamsalimu mkewe, akafululiza msalani akaoga

***Ka- mfululizo wa vitendo/utokeaji wa vitendo vingi kwa wakati mmoja.***

(n) Akifisha sentensi hii: (al 2)

Mmea wa pareto ni muhimu mno nchini akasema afisa wa kilimo

***"Mmea wa pareto ni muhimu mno nchini," akasema afisa wa kilimo.***

(o) Badilisha katika usemi wa taarifa: (al 2)

"Tutakusaidia ikiwa utashirikiana nasi," afisa wa usalama akasema.

***Afisa wa usalama alisema kuwa wangemsaidia ikiwa angeshirikiana nao.***

(p) Andika katika ukubwa ukizingatia neno lililopigwa mstari. (al 1)

Aliyerembesha uso kwa poda.

***Aliyerembesha juso kwa poda.***

(q) Bainisha maana mbalimbali za sentensi ifuatayo: (al 3)

Mwalimu amempigia wanafunzi simu

***i) Ametumia simu kama chombo kumpiga mwalimu.***

***ii) Amepiga simu kwa niaba ya mwanafunzi.***

***iii) Amempiga kwa sababu ya simu.***

***iv)***

(r) Silabi mwambatano ni nini? (al 1)

***Ni silabi ambayo ina muundo wa zaidi ya konsonanti moja***

(s) Tunga sentensi moja udhihirishe maana mbili za neno hili: Rudi (al 1)

***Rudi – adhibu mwana***

***Rudi – Rejea***

(t) Pigia mstari vivumishi katika sentensi ifuatayo kisha uandike aina yake. (al 2)

Bibi huyu ni mpole uso wake wenye haya huuinamisha kila mara.

Huyu – Kivumishi kiashiria.

Wake – kivumishi kimilikishi.

Wenye – Kivumishi cha pekee.

**ISIMU JAMII**

Maenezi ya Kiswahili Afrika Mashariki punde baada ya uhuru yalikuwa na chagamoto tele. Fafanua zozote tano. (al 10)

**(a) Uhaba mkubwa wa wataalamu wa Kiswahili**

**(b) Athari  kutoka kwa lugha ya kwanza.**

**(c) Watu kuchangamka lugha nyinginezo ka vile kiingereza, kijerumani.**

**(d) Imani potovu – lugha ya Kiswahili ni duni**

**(e) Uhaba wa walimu wa Kiswahili.**

**(f) Uhaba wa vitabu vya Kiswahili.**

**(g) Kutokuwepo kwa sera ya lugha kutoka kwa baadhi ya serikali za mataifa ya Afrika mashariki.**

**(h) Uhaba wa pesa za kutafikia**

**(i) Nchi za Afrika za kukuza na kuendeleza Kiswahili**

**Zozotte 5 x 2 = 10**

**Lazima afafanue.**

**PAPER 3**

**MARKING SCHEME**

1. Msemaji – Dora
   Msemewa – mwalimu majisafu
   Mahali – nyumbani kwao
   Sababu – Kutelekeswa kwa kazi zote za kuwalinda wanao walemuvu bila usaidizi wa mumewe majisifu. (1 x 4)

   (b) Utohozi – Petroli
   Swali balagha : "wewe unafikiri ninatumia petrol nini? (2 x2)

   (c) Migogoro

(i) Migogoro ya kindugu

Bwana mtemi na familia yake wanakinzana. Madhubuti amekuwa mwasi kwa babake. Mtemi na mkewe wanasomeana kila mara. Mtemi pia anashiriki mapenzi nje ya ndoa.

Bwana majisifu na mkewe dora vile vile wana migogoro kuhusu ulezi wa wanao vilema.

(ii) Migogoro kati ya watawal na watawaliwa

Mtemi na nduguye hawapikiki chungu kimoja. Wao wanazomeana kila mara. Hali inayowafanya wasiwasiliane ufanisi au matatizo yao.

(iii) Migogoro kati ya watawala na wataliwa

Mzee matuko weye anatiwa nguvuni kwasababu ya kumwambia mtemi wazi wazi kuwa utawala wake ni mbaya na anafua kuondoka uongozini. Mtemi anawadhuklumu wanasokomoko kwa kunyakua shamba zao kama ule la chichiri Hamadi.

(iv) Migogoro ya waajiri na waajiriwa

Mtemi Nasaba bora anawaajhiri na kufata kazi wafanya kazi wakati wowote. Akiona wanafanya kazi vyema anawapiga kalamu. Wafanyakazi wengi sokomoko wanafanya kazi za sulubu zilizo na mishahara ya kijungu jiko.

(v) Migogoro ya mashamba

Wanasokomoko na Tomoko kwa ujumla wanamlaumu mtemi kwa kuwapokonya mashamba yao. Amani hana furaha kwa sababu ya shamba lao kuchukuliwa na Bwana Mtemi.

(vi) Migogoro ya kimapenzi

Majununi na mitchelle wamekuwa na huba. Hata hivyo Mitchelle anamkataa majununi kwa kusingizia nyumba. Mashaka anaamua kutotoka shuleni kwa sababu ya mapenzi yake kuvunjika.

Mengine

(vii) Migogoro ya kinasaba

(viii) Migogoro ya kijinsia

(ix) Migogoro ya askari na wanachi

(x) migogoro ya setka katika uandishi

(xi) migogoro ya elimu

1. Wanasokomoko wanapokonywa mashamba

   Mtemi anampokoonya chichir Kamadi shamba lake la ekari mla mbili sabini. Alichukuwa shamba lake marehemu mwinyi hatika mtembezi. Na pia alipofanya kazi katika wazara ya Ardhi na makao aliweza kutendeneza hatimiliki bandia za mashamba.

2. Kuuawa na viongozi

   Mtemi aliwahonga majambazi ili waweze lumuua chichir hamadi iliaweze kuchukua shamba lake. Askari waliobimwa na mtemi walimpiga mamake Imani na kusababisha kifo chake.

3. Wanarochi wanadhulimimiwa kupita ufisadi

   Mtemi pamoja na wasimamizi wanabumia pesa zilizotaliwa kujenga hsopitali kujenga zahanati na kasha kujifaidi na pesa hizo mifukuni mwao.

4. Yusuf anadhulumiwa kwa kufungwa kifungo cha maisha kwa kusingiziwa kumuua babake chichir Hamadi.

   Amani na Imani wanafungwa kwa kusingiziwa kumuua kititi uhuru.

5. Waandishi wanadhulumiwa kwa kuibiwa miswada yao kwa njia za kilaghai na watu amabo hawana vipawa. Amani anaibiwa mswada na mwalimu majisifu.

6. Wagonjwa zahanitini wanadhulumiwa kwa kutopewa huduma bora pale zahanitini. Wauguszi ni wazembe kazini, wanawadhihaki na kukejeli wanaowaleta wagonjwa wao mfano Amani na Imani wanapompeleka kitoto Uhuru.

7. Wananchi wanalazimishwa kutoa ngeje za kuwapeleka watoto wa viongozi kusomea ughaibuni. Mtemi analazimu wanasokomoko kutoa pesa za mwanake kwende kusomea ughaibuni.

8. Waajiri wanawadhulumu waajiriwa kwa kuwapa kazi za sulubu ambazo malipo yake ni ya kijingujiko. Mtemi anampiga fagio mfanyikazi wake. Amani anatanya kazi ya kukama ng'ombe nk.

9. Wakoloni wanawadhulumu waafrika walipokuwa barani Afrika. Waafrika hawakuruhusiwa kupanda mimea iletayo fadha na figuo wa gredi.

10. Vyombo vya dola vilivyochini ya utawala mbaya wa mtemi unawadhuluma watu. Askari wanawapiga na kudhulumiwa watu wasiokuwa na hatia mamake Imani anaaga kutokana na kichapo cha Askari.

1. (a) (i) msemaji ni mzee babu
 (ii) msemewa ni wanatekede
 (iii) mahali kwa mzee babu
 (iv) sababu walikuwa wamekusanyika kwa mzee babu ili wafumbuliwe fumba la matatizo yanayowakumba.

(4 x 1 = 4)

(b) (i) Ni msiri – Alijua mengi lakini aliyatoa kwa njia ya hadithi mafumbo na ushairi
 (ii) ni mwenye busara – Anahifadhi mavuno anyayoletewa ili kuwafaa wanakijiji hao wakati wa upungufu wa chakula.
 (iii) ni mwenye mawazo mapevu – Anawambia wanakijiji kwamba si kila panapo mawingu meusi na mazito mvua hunyesha.
 (iv) ni mzalendo – Anakipenda kijiji chake ndio maana anashirikiana na wenzake kutafuta suluhisho.

(za kwanza 4 x 1 = 4)

(c) Jazanda / istiara (al 1 x 2 = 2)

Mifano

Hadithi ni ya Kobe na ndege
(a) Kobe anawakilisha viongozi wenye tama na ubinafsi kama vile Bwana Mtajika. Kobe ananyakua vyote anavyopewa huko mbinguni.
(b) Kobe pia anawakilisha viongozi wanjanja na wanafiki kama vile Bwanan Mtajika na Mchupa. Kobe anajifanya mwema anachangiwa manyoya na ndege kasha anawasaliti.
(c) Kobe anaonyesha ubaguzi wa viongozi – Anakula kwanza na kuwapa ndege makombo.

(d) Kobe kuanguka ardhini ni luonyesha kuanguka kwa uongozi mbaya. Uongozi wa Bwana Mtajika unaporomoka.
(e) Ndege kumchangia Kobe manyao ni ishara ya ushirikina wa wanatekede kupinga kura na kumwezesha kupata mamlaka.
(f) Kupewa makombo kwa ndege inaonyesha dhuluma wanazopata wanyonge.
(g) Ndege kuchukua / kumnyang'a Kobe manyoa inaonyesha nguvu walizonaza wanyonge.
(zozote 5 x 2 = 10)

<u>Ubinafsi:</u>

(i) mapenzi kati ya Chritine and Peter yanalenga mahitaji yao ya kibinafsi.
(ii) Peter aliwapunja wavuvi pesa ili ajinufaishe yeye mwenyewe akiuza samaki ghali huko ng'ambo.
(iii) Christine anatamani kuolewa katika familia ya kitajiri. Anajiona kama ng'ombe wa kizungu kwa vile amesome.
(iv) Chrisitne hamuulizi Peter kuhusu msichan anayetembea naye kwa kuhofia kukitia mchange kitumbua cha uhusiano wao.
(v) Peter aliwapenda wasichana ili kutimiza haja zake kimwili sio kuwaoa.
(vi) Peter alijitia kuwahurumia wafanyikazi wake bure, alitaka tu wamzalishie mali.
(vii) Peter alijitia kumpenda Zac hata akiwa na hali yake ya kimaskini ili afanyiwe kazi na aletewe wasichana.
(zozote 5 x 2 = 10)

<u>Ushirikina</u>

(i) Msoi anaamini ndoto anazoota kuwa ziliandama na matukio fulani. Ndoto zake ziliaminika kuwa za kweli.
(ii) Msoi aliamini kuwa lazima kungekuwa na kitu kibaya amabcho kingetokea katika Baa hiyo ya Makaburini.
(iii) Alipojikwa na bakuli lake la maua lilivunjika vipande vipande aliamini iliashivia mkosi ambao ungetokea, aliamini ilikuwa kama anakanywa.
(iv) Kubana kidole chake mlangoni mwa gari aliamini ni onyo la kutoenda huko walikokuwa wanaenda kwani kungetokea balaa.
(v) Alikuja kuichukia Baa la Makaburini kw akuwa ilikuwa karibu na makaburini au mavani Alililisi kungekuwa na mkosi.
(vi) Akiwa kwenye baa anabadili mtindo wake wa kukaa wa kawaida anaangalia upande wa makaburini akidhani ndoto yake ingetabirika wakati wowote.
(vii) Kutumbua macho kulionyehsa kuwa sasa mambo aliyotabiri yamewadia alipoona vizuu.
(zozte 5 x 2 = 10)

**MSTAHIKI MEYA**

(a) Msemaji – Waredi
Msemewa – Siki

Mahali – Zahanatini
Lini

(b) Tabaini – Ni mbinu ambayo
(c) Msemaji ni Waridi
   (i) anashawishika kwa haraka – Anaamini yale wanayosema wanasiasa, vyombo vya habari na wasomi eti nchi yake ni maskini
   (ii) Mwenye kiburu – Anamkaripia mama Dddavue kaole kwa maneno makali bila kujali hali ya motto wake. Pia mkali / mgomvi.
   (iii) Mtiifu – Anafuata maagizo ya kutowatibu watu wasio na fedha.
   (iv) Mtamaushi – Anaamua kuacha kazi baada ya kuona kuwa mazingira na hali ya kazi hayabadiliki.
   (v) Mbinafsi – Hakuwafikiria wagonjwa wake anapoamua kuacha kazi zahanatini.
   (vi) Ana msomamo thabiti – Anaamua kuacha kazi baada ya kuona hali mbaya ya kazi.
   (vii) Mwoga – Anaogopa anaposikia fununu za mgomo wa maandamano.

(Mwanafunzi ataje sifa na kuidhibitisha)
(Maelezo yaelekeana na sifa)

<u>Umaskini</u>

(a) Baraza haliwezi kutoa huduma bora kw awanacheneo – maji safi
   - Usafi w mazingira km takataka
   - Dawa zahanatini
(b) Mchi kutegemea mataifa ya kibepari kwa mikopo.
(c)Baraza kushindea kulipa mishahara kwa wakati, wanaicheleweshа na hata wakati mwingine kupila nusu. Barasa limefilisishwa na wizi / ubadhirifu wa Meya na Washauri wake.
(d) Wagonjwa zahanatini hawawezi kugharimia matibabu yapo. Hawana hata karatasi za kunakilia uabalesio wao.
(e) Wafanyikazi wa Baraza kutembea kwa miguu na kwa masaa mengi kufika kazini kwani hawana nauli.
(f) Wafanyikazi wanakosa pesa za kununua chakula wala makombo kinachowadhuru.
(g) Wanakopsa pesa za kugharimia mahitaji ya kimsingi – makao, kiberiti ili kutokosa chakula.
(h) Watoto wao waugua magonjwa yasababishwayo na ukosefu wa lishe bopra – utapia – mlo

(zozote 5 x 2 = 10)

Matumizi ya mbinu ya majazi katika mstahiki Meya

(a) Bwana sosi – Kukotana na neno la kiingere za:
   (i) 'source' – chanzu cha yeye ndiye chanzo cha matatizo mengi ya wanachenea
   (ii) 'Source" – kutia ladha. Maisha ya vibaraka wake yalipata ladha kwa kupewa mishahara ya juu na marupurupu mengine.

(iii)Aina ya msimu – 'sosi' unao – maarisha kula. Alikuwa mlafi. Pia alitumia cheo chake kula na kujitajirisha na mali ya wanacheneo.

(b) Mstahiki Meya - Alistahikli kuondolewa mamlakani kwa kuwatesa wananchi.
- Alistahiki kulaumiwa kwa matatizo ya wanacheneo

(c) Bwana uchumi n akazi – maswala ya kiuchumi na kazi Barazani.

(d) Bwana usalama – alishughulika na usalama.

(e) Bwanan uhusiano mwema – alihakikisha kulikuwa na uhusiano mwema baina ya cheneo na majirani / nchi za nje.

(f) Siki – Msikivu - alisikiliza sana matatizo ya wanachi
- kinwaji kikali / kinawasha ulimi – alimghasi Meya kuboresha hali za maisha za wanacheneo.

(g) Bili – Orodha ya vitu pamoja na malipo yake. Yeye ndiye aliyepanga orodha za njia za kupora baraza.

(h) Waredi – Ua linalovutia lakini linalokauka mara linapotolewa mtini.
Anajaribu juu chini kuwapa matumaini wagonjwa zahanatini lakini ajuapo ukweli anajiuzulu ghafla.

(i) Tatu – Anajaribu juu chini kuona matatiz ya wafanyikazi yametatutliwa.

(j) Beka – Nmeo la kuitikia hasa kwa wanawake. Aliitikia wito wa kutetea maslahi ya wafanyikazi.

(k) Cheneo – Kitu kilichoenea

(l) Kajifahari – samaki mkubwa kuliko kamba
- Mkahawa mkubwa tena wa kifahari.

(m)Shuara – Mji mdogo jirani – Mambo huko yalikuwa shwari.

(n) Kheri – Ana heri yaani mwenye amani, utulizu na salama.

(zozote 10 x 2 = 20)